# HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA TANGA MHE. WAZIRI KINDAMBA KATIKA HAFLA YA UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA WALIMU WA TAALUMA MKOA WA TANGA KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 50 YA NECTA YALYOFANYIKA UKUMBI WA SHULE YA SEKONDARI GALANOS TAREHE 09/11/2023 SAA 2 :30 ASUBUHI

- **Dkt. Said Ally Mohamed, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania;**
- **Katibu Tawala, Mkoa wa Tanga;**
- **Afisa Elimu wa Mkoa wa Tanga;**
- **Afisa Elimu wa Jiji la Tanga;**
- **Wawezeshaji wa Mafunzo - Maafisa Mitihani toka NECTA;**
- **Ndugu Walimu wa Taaluma toka shule za Msingi na Sekondari za Mkoa wa Tanga;**
- **Ndugu waandishi wa Habari, Mabibi na Mabwana;**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania......**.

**Ndugu washiriki**;

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kujumuika nanyi katika mafunzo haya yenye nia ya kuboresha utendaji kazi ya Utahini katika ngazi ya shule, hatimaye kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na tathmini endelevu ngazi ya shule. Pia, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajalia afya njema na kuweza kushiriki katika mafunzo haya muhimu kwa Taifa letu.

Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo haya. Niwapongeze Baraza la Mitihani la Tanzania kwa kuandaa Mafunzo haya yenye lengo la kuwezesha Walimu wa Taaluma kwa shule za Msingi na Sekondari Mkoa wa Tanga kuhusu masuala ya msingi katika utahini ili wakawawezeshe walimu wenzao katika shule zao. Hii ni heshima kubwa kwa Mkoa wa Tanga na kwa niaba ya wadau wote wa elimu natoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Baraza.

Nawapongeza viongozi wa Elimu wa Mkoa wa Tanga kwa kufanikisha maandalizi yote muhimu ya mafunzo haya na kuhakikisha walimu walioalikwa wanaitikia wito na kuhudhuria kwa wakati. Pia nawapongeza walimu wote mlioteuliwa kushiriki mafunzo haya.

**Ndugu washiriki**;
Baraza la Mitihani ni Taasisi muhimu katika Taifa letu kutokana na dhamana iliyopewa ya kusimamia tathmini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama Katibu Mtendaji wa Baraza alivyoeleza mwezi Novemba mwaka **2023** Baraza linafikisha miaka **50** tangu kuanzishwa kwake. Nalipongeza Baraza la Mitihani kwa kufikisha miaka **50**. Kwa kipindi chote hiki, Baraza limekuwa na mchango mkubwa katika kutoa mwelekeo wa Elimu katika Nchi yetu. Wengi wetu tulipo hapa ni matunda ya Baraza letu la Mitihani.

Baraza la Mitihani limekuwa imara katika Uendeshaji wa Upimaji na Mitihani katika Mikoa yote Tanzania kwa kushirikiana na Kamati za Mitihani za Mikoa. Ushirikiano uliopo kati ya Baraza na Kamati za

Mitihani za Mikoa umewezesha Uendeshaji na Upimaji wa Mitihani kufanyika kwa ufanisi mkubwa. **Hongereni sana**.

**Ndugu washiriki;**

Mafunzo yanayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania yanatarajiwa kuwaongezea walimu ujuzi kuhusu jinsi ya kuandaa maswali yanayopima umahiri. Ujuzi mtakaoupata utawawezesha kuandaa maswali bora katika kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Pia kuweza kubaini mahiri walizopata wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mtaweza kuchukua hatua muhimu za kusaidia wanafunzi kuimairika zaidi katika maeneo yaliyobainika kuwapa changamoto wakati wa ujifunzaji. Hatua hizo ni pamoja na kufanya ufundishaji rekebishi.

**Ndugu Washiriki**;

Pamoja na mafunzo kuhusu namna bora ya kuandaa maswali pia mtajadili kuhusu mada zinazowapa wanafunzi changamoto kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021 na hatua za kuchukua katika kuwezesha wanafunzi kujifunza mada hizo. Lengo la majadiliano hayo ni kupata mbinu mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi namna ya kujifunza mada husika na kuwezesha kujifunza vizuri zaidi. Majadiliano hayo yatawaimarisha zaidi na mtakuwa mahiri katika ufundishaji na kufanya tathmini bora za mada hizo. Kwa kufanya hivyo, Baraza la Mitihani litaweza kupata alama endelevu za wanafunzi shuleni zenye kuaminika zaidi kwasababu kutakuwa na usawa kati ya mitihani na majaribio yanayotolewa shuleni pamoja upimaji na mitihani ya mwisho inayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

**Ndugu washiriki;**

Matokeo bora ya ujifunzaji yaliyowekwa katika mitaala yetu yatawezesha Taifa kuwa na watu walioelimika, mahiri na wabunifu kuelekea uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Hivyo ni muhimu kuwa na upimaji na tathmini sahihi unaolenga kumpima mtahiniwa katika nyanja zote.

Nitoe wito kwa Walimu mliopata nafasi hii kuitumia vizuri kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania ili siku mbili za mafunzo ziweze kuacha alama katika Mkoa wa Tanga. Aidha, baada ya mafunzo kuutumia ujuzi mliopata kuimarisha utendaji kazi hasa katika tathmini kwenye maeneo yenu ya kazi. Kwa vile Mkoa una walimu wengi wanaohitaji kupata mafunzo haya, **nitoe wito kwa Afisa Elimu Mkoa** kuhakikisha mpango unaandaliwa ili walimu wa taaluma watumike kutoa mafunzo haya kwa walimu wote wa Mkoa wa Tanga ambao hawakupata fursa hii kwa kuanza na shule wanazofanya kazi.

**Ndugu washiriki;**

Kama Mkoa, tunaahidi kusimamia lengo jema la Baraza kwa walimu wanaopewa mafunzo haya kuyafikisha kwa walimu wengine waliopo katika shule mbalimbali za Mkoa huu wanaofundisha masomo mbalimbali ili kuwaimarisha katika Nyanja ya utahini. Tunaamini kwa kufanya hivyo, maswali ya mitihani na majaribio yanayofanywa katika shule yatakuwa na viwango vinavyohitajika hivyo kupima wanafunzi katika viwango vinavyotakiwa na hatimaye kuwa na watahiniwa walioandaliwa vyema kabla ya upimaji na mitihani ya Taifa.

**Ndugu washiriki;**

Mwisho napenda kuwashukuru wote mliohudhuria na nawatakia mafunzo mema yenye kuleta ufanisi katika utendaji kazi wenu wa kila siku. Aidha, mafanikio ya mafunzo haya ni pale mtakapofikisha umahiri mtakaoupata kwa walimu na kusimamia vyema utekelezaji wake.

Baada ya kuyasema haya, natamka kuwa mafunzo kuhusu taratibu za kuzingatia katika Utunzi wa maswali ya Mitihani unaozingatia umahiri pamoja na tathmini ya mada zilizobainika kuwapa watahiniwa changamoto yamefunguliwa rasmi**.**

***Ahsanteni kwa kunisikiliza.***